



ST. JOSEPH IKELU COLLEGE OF HEALTH AND ALLIED SCIENCES (IKELU-COHAAS)

P.O. Box 929 MAKAMBAKO, TEL. +255 790 950 915

Email: info@ikelucohas.com

Makambako, Njombe, Tanzania.

MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MUUNDO WA ADA (FEE STRUCTURE) KOZI YA STASHAHADA YA UUGUZI NA UKUNGA (DIPLOMA IN NURSING AND MIDWIFERY) KWA MWAKA WA MASOMO WA 2026/2027

Chuo cha St. Joseph Ikulu kimesajiliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) kwa namba ya usajili **REG/NACTVET/1190**. Programu ya mafunzo inayotolewa kwa sasa ni Stashahada ya Uuguzi na Ukunga (Diploma in Nursing and Midwifery).

I. MAHALI CHUO KILIPO

Chuo cha St. Joseph Ikulu kipo katika Halmashauri ya Mji Makambako, Mkoa wa Njombe, umbali wa takriban kilomita 18 kutoka Kituo cha Mabasi cha Makambako, kwenye barabara ya Makambako–Songea.

II. NAMNA YA KUFIKA CHUONI

Wanaotoka mikoani washuke kituo cha Ikulu Hospital.

III. TAREHE YA KUANZA USAJILI NA KURIPOTI

Usajili ulianza mwezi Mei 2026, na tarehe ya kuripoti chuoni ni mwezi Oktoba 2026.

Ukifika, ripoti katika ofisi ya utawala ya chuo ukiwa na vitu vifuatavyo:

- Nakala ya Cheti cha Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE) au hati ya matokeo (result slip).
- Nakala ya Cheti cha Kuzaliwa au Hati ya Kiapo.
- Picha nne (4) za hivi karibuni za ukubwa wa pasipoti, zenye mandharinyuma ya rangi ya bluu.
- Fomu ya maelekezo ya kujiunga iliyojazwa kikamilifu.
- Fomu ya Uchunguzi wa Afya iliyojazwa kikamilifu.
- Hati ya matokeo, barua ya mapendekezo na vyeti (kwa wanafunzi wanaopanda ngazi hadi NTA Level 6).
- Rimu mbili (2) za karatasi za A4 kwa muhula (rimu nne kwa mwaka).
- Hati ya malipo ya benki (bank pay-in slip) inayoonesha malipo ya ada na ya michango mingine.

Notisi Muhimu: Kutoa taarifa za uongo au hati bandia ni kosa la jinai na kunaweza kusababisha hatua za kisheria.

1.0 MAELEZO KWA UJUMLA

- A. Malipo yote yafanyike kupitia **Benki ya CRDB**. Akaunti ya chuo imeainishwa kwenye majedwali yanayoonesha namna malipo yanavyofanyika, na utawasilisha risiti halisi chuoni katika ofisi ya Mhasibu.
- B. Ufikapo chuoni unatakiwa uwe umelipa ada kama ilivyoainishwa kwenye **Jedwali Namba 04** na michango ya mwaka husika kama ilivyoainishwa kwenye **Jedwali Namba 05**.
- C. Ada haitabadilika katikati ya mwaka wa masomo, lakini inaweza kubadilika mwanzoni mwa mwaka wa masomo unaofuata kutegemeana na mabadiliko ya gharama za kuendesha mafunzo.
- D. **Sare:** Kaunda suti 1, gauni 1 na T-shirt 1, vyote vinapatikana chuoni. Mwanafunzi akihitaji kuongeza jozi nyingine ya sare atapaswa kushona kulingana na mwongozo uliowekwa, unaopatikana katika ofisi ya malezi ya

wanafunzi.

- E. Kabla ya kufika chuoni kila mwanafunzi atapaswa kufanyiwa uchunguzi wa afya na kujaza fomu maalumu ya kitabibu (Medical Examination Form).
- F. Wanafunzi wote wa mwaka wa kwanza watalazimika kuishi katika hosteli za chuo bila gharama yoyote.
- G. Mwanafunzi wa mwaka wa pili na wa tatu anaruhusiwa kuishi kwenye hosteli zilizopo ndani au nje ya chuo.
- H. Mwanafunzi wa mwaka wa tatu atajitegemea gharama za utafiti.
- I. Endapo mwanafunzi atashindwa kufikisha wastani wa alama zinazotakiwa kwenye mtihani wa majaribio kwa nusu au zaidi ya moduli anazosoma, gharama ya kurudia mitihani hiyo ni Tsh. 30,000/= kwa masomo ya nadharia na Tsh. 30,000/= kwa masomo ya vitendo. Endapo atashindwa pungufu ya nusu ya moduli za nadharia au vitendo, gharama ya kurudia mitihani hiyo ni Tsh. 10,000/=.
- J. Endapo mwanafunzi atashindwa mtihani wa kumaliza muhula wa kwanza au wa pili, gharama ya kurudia mtihani huo ni Tsh. 100,000/= bila kujali idadi ya masomo aliyoshindwa.
- K. Endapo mwanafunzi hatafanya mtihani wa majaribio unapofanyika kwa mara ya kwanza na akaomba kufanya mtihani maalumu (Special Examination), gharama ya kufanya mtihani huo ni Tsh. 100,000/= bila kujali idadi ya masomo ambayo hakufanya.
- L. Wanafunzi wote wanapaswa kuwa wanachama hai wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) au bima nyingine ya afya inayokubalika katika hospitali za umma na binafsi. Wanafunzi wasio na bima hai ya afya watapaswa kuchangia kiasi cha Tsh. 50,400/= kila mwaka.
- M. Kwa wanafunzi watakaowasilisha maombi ya kujiunga na NHIF, kadi zao za bima zitakuwa tayari ndani ya siku thelathini (30) tangu kusajiliwa chuoni na kuwasilisha maombi hayo.
- N. Kila mwanafunzi aliyefikisha umri wa miaka 18 anatakiwa kuwa na Namba ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA) kwa ajili ya usajili wa Bima ya Afya (NHIF).

2.0 MAHITAJI BINAFSI YA MSINGI

- A. Shuka 4, blanketi 1, mto na foronya, taulo, nguo za michezo, sweta jeupe lisilo na maandishi, ndoo ya kuogea, chandarua, soksi nyeupe (wasichana na wavulana), na viatu vyeusi vya kufunika miguu. Viatu visiwe vya wazi (open shoes), visiwe na visigino virefu, wala visipige kelele wakati wa kutembea.
- B. Madaftari makubwa (counter books). Mwanafunzi anashauriwa pia kuwa na simu janja (smartphone) au kompyuta mpakato (laptop) kwa ajili ya kujisomea.
- C. Fedha za matumizi madogo madogo akiwa chuoni, pamoja na fedha ya chakula. Huduma ya chakula inatolewa na mzabuni kwenye cafeteria iliyopo chuoni kwa gharama ya kuanzia Tsh. 1,500/=.

**SEHEMU A: GHARAMA ZA MAFUNZO — UUGUZI NA UKUNGA (NURSING AND MIDWIFERY)
KWA MWAKA WA MASOMO WA 2026/2027**

JEDWALI NAMBA 01: ADA NA MICHANGO MINGINE YA CHUO (TSH)

Na.	Maelezo	Mwaka I	Mwaka II	Mwaka III
1.	Ada	1,000,000	1,100,000	1,200,000
	MICHANGO MINGINE			
1.	Computer Lab	150,000	150,000	150,000
2.	Mitihani ya ndani	200,000	200,000	200,000
3.	Usajili	20,000	20,000	20,000
4.	Cheti cha kuhitimu (Leaving Certificate)	-	-	20,000
5.	Huduma za Maktaba	20,000	20,000	20,000
6.	Mahafali (pamoja na joho)	-	-	85,000
7.	Mafunzo kwa vitendo (Field work)	-	130,000	-
8.	Usimamizi wa utafiti (Research supervision)	-	-	50,000
9.	Bima ya afya (kwa wasiokuwa nayo)	50,400	50,400	50,400
10.	Michezo	10,000	10,000	10,000
11.	Fedha ya uendeshaji wa serikali ya wanafunzi (IKELU-COHAS Student Organisation Fee)	10,000	10,000	10,000
12.	Kitambulisho	10,000	-	-
13.	Vitabu vya mazoezi	80,000	-	-
14.	Sare (gauni 1, Kaunda suti 1, T-shirt 1)	65,000	-	-
15.	Hospital clinical rotations	200,000	200,000	250,000
	Jumla	1,815,400	1,890,400	2,065,400

JEDWALI NAMBA 02: MICHANGO MAALUMU (TSH)

Na.	Maelezo	Mwaka I	Mwaka II	Mwaka III
1.	NACTVET Quality Assurance	20,000	20,000	20,000
2.	Ada ya Mitihani ya Wizara ya Afya	150,000	150,000	150,000
3.	Mchango wa CSSC	5,000	5,000	5,000
	Jumla	175,000	175,000	175,000

JEDWALI NAMBA 03: JUMLA YA ADA NA MICHANGO (TSH)

Muhula	Mwaka I	Mwaka II	Mwaka III
Muhula wa I	1,105,400	1,155,400	1,155,400
Muhula wa II	885,000	910,000	1,085,000
JUMLA KUU	1,990,400	2,065,400	2,240,400

SEHEMU B: VIFAA VYA KUTUMIA WAKATI WA MAFUNZO

- | | |
|---|----------------------------|
| i. Utepe wa kupimia (MUAC tape measure) — kwa mwaka wa pili | iv. Clinical thermometer 1 |
| ii. Blood pressure machine 1 | v. Fetoscope |
| iii. Clean gloves, boksi 1 kila anapoanza mwaka wa masomo | vi. Sphygmomanometer |
| | vii. Scientific calculator |
| | viii. Stethoscope |

JEDWALI NAMBA 04: MALIPO YA ADA (TSH)

Namna ya kulipia ada	Mwaka I	Mwaka II	Mwaka III
MUHULA WA KWANZA			
Awamu ya 1 — 1/10/2026	250,000	275,000	300,000
Awamu ya 2 — 1/1/2027	250,000	275,000	300,000
MUHULA WA PILI			
Awamu ya 3 — 1/4/2027	250,000	275,000	300,000
Awamu ya 4 — 1/6/2027	250,000	275,000	300,000
JUMLA	1,000,000	1,100,000	1,200,000

CRDB BANK — AKAUNTI NAMBA 10361260061**Jina la Akaunti: ST.JOSEPH COLLEGE OF HEALTH AND ALLIED SCIENCES****JEDWALI NAMBA 05: MALIPO YA MICHANGO (TSH)**

Namna ya kulipia michango	Mwaka I	Mwaka II	Mwaka III
MUHULA WA KWANZA			
Awamu ya 1 — 1/10/2026	450,000	425,000	400,000
Awamu ya 2 — 1/1/2027	155,400	180,400	155,400
MUHULA WA PILI			
Awamu ya 3 — 1/4/2027	385,000	360,000	485,000
JUMLA	990,400	965,400	1,040,400

CRDB BANK — AKAUNTI NAMBA 10361260061**Jina la Akaunti: ST.JOSEPH COLLEGE OF HEALTH AND ALLIED SCIENCES****NB:**

- i. Ndugu Mzazi/Mlezi/Mfadhili, hakiki akaunti vizuri kadiri jedwali lilivyoainisha. Akaunti ni ya CRDB BANK na jina lake linasomeka: ST.JOSEPH COLLEGE OF HEALTH AND ALLIED SCIENCES.*
- ii. RISITI ZA MALIPO ziandikwe jina kamili la mwanafunzi. RISITI ZA MALIPO zenye majina ya wazazi/walezi/wafadhili HAZITAPOKELEWA.*
- iii. FEDHA IKISHAWEKWA KWENYE AKAUNTI HAITAREJESHA.*

.....

Charles Magwaza
MKUU WA CHUO